

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI

Simu: +2552629633
Nukushi: +255 262 963 316
Barua pepe: km@ardhi.go.tz
Tovuti: www.ardhi.go.tz



Mji wa Serikali Mtumba,
S.L.P. 2908,
40477- DODOMA

TAARIFA KWA UMMA

KUHUSU UMILIKISHAJI ARDHI KWA VIWANJA VILIVYOPIMWA PAMOJA NA
ULIPAJI WA KODI YA PANGO LA ARDHI

Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi inakumbusha umma kwamba ni wajibu wa kisheria kwa wale ambao ardhi zao zimepangwa na kupimwa kuwasilisha maombi ya kumilikishwa ardhi kwa Kamishna wa Ardhi kwa ajili ya kumilikishwa. Aidha, wamiliki wa ardhi wanakumbushwa wajibu wao wa kisheria wa kulipa kodi ya pango la ardhi.

Kwa Tangazo hili, Wizara inatoa muda wa siku 60 kuanzia tarehe 5/2/2022 ya kuhakikisha kuwa wale waliopimiwa viwanja wanawasilisha maombi ya kumilikishwa, na wale wenye milki za ardhi wawe wamelipa kodi ya pango la ardhi.

Mmiliki ambaye hatalipa kodi ndani ya muda uliotolewa, Serikali itachukua hatua za kisheria ikiwemo kufuta umiliki, kupiga mnada na kumilikisha viwanja vilivyopimwa kwa wananchi wengine wenye uhitaji. Zoezi hili litaanza rasmi tarehe 6/4/2022.

IMETOLEWA NA

A handwritten signature in black ink, appearing to be 'M. M. M.' or similar.

KATIBU MKUU
WIZARA YA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI
4 Februari 2022